TANGAZO LA SERIKALI NA. 756 la tarehe 30/8/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA NYAMSWA YA MWAKA, 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa eneo la Nyamswa ya mwaka, 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika Eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NMS1 yenye majira – nukta 590391MS, 9704367.43KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS84$^{0}$53'30"MG kwa umbali wa kilomita 0.18 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NMS2 yenye majira – nukta 590213.14MS, 9707351.53KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea

Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ317$^{0}$10'49"MG kwa umbali wa kilomita 0.32 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NMS3 yenye majira – nukta 589999MS, 9707582.62KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ14$^{0}$31'10"MS kwa umbali wa kilomita 0.613 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NMS4 yenye majira – nukta 590152.47MS, 9708175.22KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa MS89$^{0}$57'11"MS kwa umbali wa kilomita 0.64 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NMS5 yenye majira – nukta 590788.69MS, 9708175.74KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS181$^{0}$43'5"KS kwa umbali wa kilomita 0.71 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NMS6 yenye majira – nukta 590767.48MS, 9707468.61KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS195$^{0}$2'35"MG kwa umbali wa kilomita 0.39 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
14 Agosti, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*